City of Dayton Department of Water

Service Line Compliance Program

# Arifa ya Huduma ya Mabomba Yenye Risasi

Mpendwa Mtumiaji:

Idara ya Maji ya Jiji la Dayton ndiyo mfumo wa maji wa umma (PWS) unaowajibika kutoa maji ya kunywa katika eneo hili. Unapokea hii arifa kwa sababu rekodi inaonyesha kuwa hii nyumba au jengo ina njia ya huduma ya mabomba yenye risasi . Huduma ya njia ni bomba linalounganisha mfereji mkuu wa maji na jengo. Maji ya kunywa ya Dayton hayana risasi, hata hivyo zile zenye njia za huduma ya risasi kwenye nyumba zao wanaweza kuathiriwa na risasi.

## Je, Hii Maana yake ni nini?

Chini ya sheria ya mamlaka ya maji Salama ya Kunywa, Wakala wa Ulinzi wa Mazingira wa Marekani (EPA) inatuhitaji sisi kuwajulisha watumiaji wa maji ambao wanahudumiwa na njia ya huduma ya GRR. Huduma ya mabomba yenye risasi ina maanisha kwamba sehemu ya bomba linalounganisha mfereji mkuu wa maji na nyumba au Jengo lina risasi.

## Nini Athari za Kiafya za Risasi?

Hakuna kiwango salama cha risasi katika maji ya kunywa. Kuathiriwa na risasi katika maji ya kunywa kunaweza kusababisha madhara makubwa kiafya kwa watu wa rika zote, hasa wanawake wajawazito, watoto wachanga (wanaonyonyeshwa maziwa ya kopo na wanaonyonyeshwa maziwa ya mama), na watoto wadogo. Baadhi ya athari za kiafya kwa watoto wachanga na watoto wakubwa hujumuisha hupungua kiwango cha IQ na kipindi cha umakini . Kuathiriwa na risasi pia kunaweza kupelekea kutokea kwa tatizo jipya au kulikuza tatizo lililopo la kujifunza na na tabia. Mtoto wa mtu aliyeathiriwa na risasi kabla au wakati wa ujauzito yuko katika hatari kubwa ya kuathiriwa na madhara haya ya kiafya. Watu wazima huongeza hatari ya kupata magonjwa ya moyo,shinikizo la damu, na figo au matatizo ya mfumo wa fahamuWasiliana na mto huduma wako wa afya kwa taarifa zaidi kuhusu hatari zako

## Naweza Kufanya Nini ili Kupunguza kuathiriwa na risasi iwapo Itapatikana kwenye Maji yangu ya Kunywa?

- ***Usichemshe maji kuondoa risasi.*** Kuchemsha maji hakupunguzi risasi.
- ***Safisha bomba lako ikiwa halijatumika kwa saa 6 au zaidi.*** Kiwango cha risasi huongezeka baada ya muda kadri maji yanavyokaa kwenye vifaa vya bomba vyenye risasi. Matumizi ya mara kwa mara ya maji kwenye makazi yako au jengo hupunguza kiwango cha risasi kwenye maji ya kunywa. Maji yasipotumika kwa saa 6 au zaidi, makazi au majengo yanayohudumiwa na njia ya huduma ya mabomba yaliiyotiwa risasi yanayohitaji kubadilishwa, bomba hilo linapaswa kusafishwa hadi ugundue mabadiliko ya kiwango cha joto, kisha safisha kwa dakika moja zaidi.
- ***Tumia maji ya baridi kwa kupikia, kunywa, na maandalizi maziwa ya kopo ya mtoto.*** Usipikie, kunywa au kuandalia maziwa ya kopo ya mtoto maji yanayotoka kwenye bomba la maji ya moto. Risasi huyeyuka zaidi kwa urahisi katika maji ya moto. Daima tumia maji ya baridi na pasha ikiwa inahitajika.
- **T*umia kichujio cha risasi kilichothibitishwa na ANSI.*** Vichujio vilivyoidhinishwa kwa kiwango cha ANSI/NSF 53 cha kuondoa risasi vinaweza kuwa na ufanisi katika kupunguza viwango vya risasi katika maji. Fuata maagizo ya mtengenezaji kuhusu jinsi ya kutumia mtungi ipasavyo, ikiwa ni pamoja na wakati gani wa kubadilisha kichujio. Tunapendekeza kutumia kichujio cha risasi kilichothibitishwa na ANSI/NSF 53 kwa angalau miezi sita baada ya njia za huduma kubadilishwa.
- ***Mara kwa mara safisha vichujio vya bomba la maji.*** Baada ya muda, chembe zenye risasi zinaweza kujijenga juu ndani ya skrini ya kichujio cha bomba la maji. Kusafisha kichujio mara kwa mara kutasaidia kuondoa hiki chanzo cha risasi.

DAYTON | CITY OF DAYTON water one source

320 W Monument Ave, Dayton, OH 45402

(937) 333-3725

daytonohio.gov/ServiceLineCompliance

## Naweza Kufanya Nini ili Kupunguza kuathiriwa na risasi iwapo Itapatikana kwenye Maji yangu ya Kunywa? (Inaendelea)

- ***Kwa wanawake wajamzito, watoto wachanga, na watoto wadogo.*** Baadhi ya makundi ya watu kama vile wanawake wajawazito, watoto wachanga, na watoto wadogo wanaweza kuwa hatarini zaidi kutokana na athari mbaya za risasi. Watu hawa wanaweza kufikiria kuchukua tahadhari zaidi ikiwa nyumba zao zinahudumiwa na risasi au njia ya huduma ya mabomba yaliiyotiwa risasi yanayohitaji kubadilishwa. Hizi tahadhari za ziada inaweza kujumuisha kuwa na maji yao ya kunywa yaliyochunguzwa zaidi kuhusu risasi, kutumia chanzo mbadala cha maji (kama vile maji ya chupa), au kutumia kichujio kilichoidhinishwa kwa kiwango cha ANSI/NSF 53 kwa ajili ya kuondoa risasi.
- ***Badilisha vifa vya vya mambomba vyenye risasi.*** Vichujio vingi vya zamani, valvu na vifaa vingine vya mabomba vinaweza kuwa na risasi. Bainisha ikiwa vifaa vya mambomba ya jengo lako vina risasi na badilisha wakati unaofaa.
- ***Unaweza kutamani mtoto wako apimwe  damu kwaajili ya  risasi.*** Ida ya ya afya ya kwenye kaunti yako inaweza kufikiwa kwa usaidizi zaidi.

## *Unaweza kutamani maji yako yapimwe kwa ajili ya risasi.*

Ili kuomba hili, wasiliana na Idara ya Ugavi na Matibabu ya Maji ya Dayton kwa **(937) 333-6030** au tuma barua pepe kwa **labservices@daytonohio.gov**. Hakikisha unatoa anuani yako ya barua pepe, nyumba, na namba ya simu.

Tutawasiliana nawe haraka iwezekanavyo. Kama maji yako yana ladha ya kiwango cha juu zaidi ya kile cha kawaida cha risasi, Jiji la Dayton litakupatia mtungi wa kuchujia maji bure na katriji za kubadilishia ili kuchuja maji yako.

## *Unaweza Kufanya Nini Kuhusu Huduma ya Mambomba yenye Risasi?*

Upande wa kibinafsi wa njia ya huduma inamilikiwa na kubadilishwa kwa gharama za mliki wa jengo. Jiji ya Dayton linashauri kwa nguvu zote kwamba unawasiliana na fundi bomba wenye leseni kwa kazi kwenye njia yako ya huduma. Kwa ya orodha ya hivi karibuni ya fundi bomba waliothibitishwa, tafadhali tembelea: **daytonohio.gov/691/Registered-Contractors-Lists**.

*Ikiwa hukubaliani kwamba nyumba au jengo lako halihudumiwi na njia ya huduma ya risasi, tafadhali tutaaarifu (937) 333-3725 na kamilisha utafiti wa mtandaoni wa Fahamu Mambomba yako katika* ***www.DaytonOhio.gov/KnowYourPipes****.*

Hapa wewe mwenyewe utabainisha vifaa vya mambomba ya huduma za maji ya nyumba yako na wasilisha taarifa zitakazojumuishwa kwenye kumbukumbu za njia za huduma yetu. Ili kukamilisha utafiti huu mfupi wa dakika 5 utafiti, utahitaji ya vitu vifuatavyo:

- Simu ya mkononi yenye kamera
- Sarafu au ufunguo
- Sumaku yenye nguvu ya jokofu

*Kama una maswali au unahitaji taarifa zaidi kuhusu Mpango wa Uzingatiaji Njia ya Huduma, tafadhali mawasiliano sisi katika* ***SLCP@daytonohio.gov****.*

## *Kwa Taarifa zaidi, Tafadhali Wasiliana na:*

Idara ya Maji ya Jiji la Dayton **(937) 333-3725**,tembelea tovuti ya EPA ya Marekani kwa **epa.gov/lead**, au tembelea Ohio EPA Jifunze Kuhusu Risasi/Ohio Tovuti ya Wakala wa Ulinzi wa Mazingira katika **epa.ohio.gov/monitor-pollution/pollution-issues/learn-about-lead**. Kwa maelezo zaidi kuhusu athari zingine za risasi, tafadhali tembelea tovuti ya Idara ya Idara ya Afya Sumu ya Risasi Utotoni katika **odh.ohio.gov/know-our-programs/Childhood-Lead-Poisoning**.

***Tafadhali shirikisha taarifa hii na watu wengine kwenye makazi yako au jengo, hasa wale ambao inawezekana hawakupata waraka huu moja kwa moja kwa mfano, watu katika vyumb za kupanga, nyumba ya kunyonyeshea, shule, na biashara). Unaweza kufanya hivyo kwa kubandika waraka huu kwenye maeneo ya umma au kusambaza nakala kwa mkono au kwa  au barua.***

**SKANI HAPA KWA TAARIFA YA PROGRAMU**

**Tafsiri ya hii nyaraka hii inapatikana kwa kutembelea daytonohio.gov/ServiceLineCompliance/documents.**

**Spanish:** La traducción de estos documentos se puede obtener visitando **daytonohio.gov/ServiceLineCompliance/documents** o llamando a 937-634-7835.

**Russian:** Перевод этого документа можно получить на сайте **daytonohio.gov/ServiceLineCompliance/documents** или позвонив по телефону 937-883-5987.

**Turkish:** Bu belgelerin tercümesini **daytonohio.gov/ServiceLineCompliance/documents** adresini ziyaret ederek veya 937-828-4509 numaralı telefonu arayarak edinebilirsiniz.

**Swahili:** Tafsiri ya waraka huu inapatikana kwa kutembelea **daytonohio.gov/ServiceLineCompliance/documents** au kupiga simu 937-634-7350.

**Kinyarwanda:** Ubusemuzi bw'iyi nyandiko buboneka usuye **daytonohio.gov/ServiceLineCompliance/documents** cyangwa ugahamagara 937-907-1817.